



## MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA



# Miaka minne ya Rais Samia na ukuaji wa soko la bima nchini

### Na Na Mwandishi Wetu

**K**ILA tarehe 19 ya mwezi Machi, ni kumbukumbu muhimu kwa nchi yetu, kwa kuwa taifa lilipata kiongozi mkuu, ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Machi 19, 2025 tunaadhimisha miaka minne ya uongozi wake ikiwa na mafanikio lukuku kwa ustawi wa taifa letu na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini ikiwa sehemu ya mafanikio hayo.

TIRA ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria ya Bima Sura 394.

Imepewa mamlaka ya kuratibu masuala yote ya kisera kuhusu bima ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, majukumu mengine ni kusajili na kutoa leseni kwa watoa huduma za bima, kuandaa na kutoa miongozo kwa watoa huduma za bima, kusimamia soko la bima nchini, kulinda haki za wateja wa bima na kuishauri serikali kuhusu masuala ya bima.

TIRA inajivunia uongozi makini wa Awamu ya Sita ambao umeendelea kutoa mchango kwa ukuaji wa sekta hiyo adhimi hapa nchini ukiwemo ushirikiano mahiri kutoka kwa viongozi wa juu ambao wamekuwa wakishiriki katika mikutano na midahalo mbalimbali ya Mamlaka na kutoa hotuba zenye kujenga kwa umma wa Tanzania.

Ndani ya miaka minne ya uongozi wake, TIRA imeendelea kujipambanua kama kiongozi wa mageuzi katika sekta ya bima nchini kwa kufanikisha yafuatayo :-

#### Utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, inatoa haki ya msingi ya kila Mtanzania kuwa na bima ya afya bila kujali kama wanatoka katika sekta rasmi au isiyo rasmi.

Katika kutekeleza hilo, TIRA imepewa jukumu la kisheria kusimamia skimu zote za bima ya afya ili kuhakikisha watoa huduma wanafuata taratibu sahihi za usajili wa wanachama na pia kufuatilia utekelezaji wa huduma zinazotolewa ili huduma zinazotolewa ziendelee kuwa bora na za haki kwa wanachama walio kwenye skimu husika.

Mwaka 2024, kanuni kwa ajili ya kuanza kwa utekelezaji wa sheria hiyo zimetoka ambapo zinasisitiza juu ya usajili wa wanachama kwa uwazi na kuhakikisha michango inawasilishwa kwa wakati.

Katika kuchangia juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wa kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma bora za afya, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kwa kushirikiana na wadau, imetoa kadi za bima ya afya 3,000 kwa Watanzania wenye uhitaji ikiwa ni utekelezaji wa kauli ya Kamishna wa Bima Tanzania aliyoitoa ya kuchangia kadi za bima kwa Watanzania 10,000 ili waweze kupatiwa matibabu.

#### Kuanzishwa kwa konsotia ya Bima ya Kilimo (Tanzania Agriculture Insurance Consortium)

Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu na takribani



asilimia 70 ya Watanzania wanategemea kilimo kama chanzo cha mapato.

Hata hivyo, wakulima wanakutana na changamoto kubwa za kiuchumi na mazingira, ikiwa ni pamoja na mvua za kupindukia, ukame na maafa mengine.

Takwimu zinaonesha kwamba wakulima wengi nchini wanakumbana na hasara kutokana na majanga ya asili kama ukame, mafuriko, magonjwa ya mazao na wadudu waharibifu, jambo ambalo linahitaji mfumo wa bima ya kilimo.

Bima ya kilimo inatoa fursa kwa wakulima kupunguza athari za majanga hayo na inasaidia kukuza uzalishaji wa mazao na kuimarisha uchumi wa taifa.

Konsotia ya bima ya kilimo, huwapa wakulima unafuu katika kukata bima kwa makundi, lakini kila mmoja kunufaika pale linapotokea janga.

#### Ongezeko la idadi ya Ofisi za Kanda za TIRA

Katika kuhakikisha wananchi wengi wanapata elimu ya bima, Mamlaka imeongeza wigo kwa kufungua ofisi za kanda ya Unguja na Pemba na hivyo kufanya idadi kufikia kanda 10 kwa upande wa Bara na Visiwani.

Zanzibar imeendelea kufanya vizuri katika sekta ya bima mathalani, katika Uzinduzi wa Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima kwa mwaka 2023 takwimu zilitolewa ambapo idadi ya watoa huduma wa bima kwa Zanzibar iliongezeka kwa asilimia 15 mwaka 2023 na kufikia watoa huduma za bima 92 ukilinganisha na watoa huduma wa bima 80 waliosajiliwa kwa mwaka 2022.

**Kamishna wa Mamlaka  
ya Usimamizi wa Bima  
Tanzania (TIRA), Dkt.  
Baghayo Saqware**

>> INAENDELEA UK. 5